



**Na Mzee  
Mathias Held**  
Wa Sabini

# Mfano Mzuri



**N**ilipokuwa mtoto sikuwa muumini wa Kanisa. Nilipokuwa mtu mzima na kuwa mfanya biashara ndipo nilipobatizwa.

Baba yangu alikuwa pia mfanya biashara. Alikuwa na wasiwaso sana wakati nilipojiunga na Kanisa. Alisema, "Hunywi pombe tena. Hiyo itakuwa vigumu katika mikutano ambapo kila mtu anakunywa pombe."

Lakini mimi sikuwa na wasiwaso. Niliamua kwamba wakati mtu atakaponipa pombe, ningesema, "Hapana, asante." Kisha ningeagiza kitu kingine.

Miaka ilipita, na nilifanya hivi mara nyingi sana. Baada ya muda, wafanyakazi wenzangu waligundua. Kama ningepewa pombe, wao walisema, "Mathias hanywi pombe. Mletee kitu kingine." Wengi wao zaidi waliacha kuagizia pombe pia. "Hata mimi sitaki," walisema.

Wakati mmoja wageni fulani walikuja kwenye mukutano. Wao pekee ndiyo walikuwa wanakunywa pombe.

Waliniuliza mimi, "Kwa nini hakuna mtu anayekunywa pombe? Wote ni waumini wa Kanisa lako?"

"Hapana," nilisema.

Mimi sikuwashabiria wafanyakazi wenzangu kuhusu Neno la Hekima. Nilikuwa tu thabiti katika imani yangu, na wao walitambua mfano wangu.

Wewe pia unaweza kuwa mfano mzuri. Wengine watatambua wakati unapochagua kilicho chema. Unaweza tu kuwasaidia wao kwa kuishi injili. ●

*Kutoka kwenye Mahojiano na Haley Yancey.*